

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. AB.112/353/01/53

29 Juni, 2022

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI - MARUDIO

Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti imepokea kibali cha kutekeleza Ikama na Bajeti kwa ajira mpya katika mwaka wa fedha 2021/2022 chenye kumb.Na FA.97/228/01/9 cha tarehe 13 Mei, 2022 kutoka kwa Katibu Mkuu wa, Ofisi ya Raisi Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti anawatangazia wananchi wote wenye sifa zilizoorodheshwa hapo chini kuomba nafasi hii ya Ajira.

1. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA II (RECORDS MANAGEMENT ASSISTANT II) - NAFASI MOJA (1).

(a) SIFA ZA MWOMBAJI:-

- Awe amehitimu kidato cha nne (IV) au cha sita (VI).
- Aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti "NTA level 5" mwenye cheti cha utunzaji wa kumbukumbu katika fani ya Masijala.

(b) KAZI NA MAJUKUMU YA MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU:-

- Kutafuta kumbukumbu/mafaili yanayohitajika na wasomaji.
- Kudhibiti upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu/nyaraka.
- Kuchambua, kuiboresha na kupanga kumbukumbu/nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (**classification and boxing**) kwa ajili ya matumizi ya ofisi.
- Kuweka/kupanga kumbukumbu/nyaraka katika reki (**File racks/cabinets**) katika masijala/vyumba vyya kuhifadhi kumbukumbu.
- Kuweka kumbukumbu (**barua, nyaraka nk**) katika mafaili.
- Kushughulikia maombi ya kumbukumbu/nyaraka kutoka Taasisiza Serikali.

(c) Mshahara kwa kuzingatia ngazi ya mishahara ya serikali yaani **TGS B** kwa mwezi.

2. MASHARTI YA JUMLA


- Waombaji wote wawe na umri kati ya miaka 18 hadi 45

- Waombaji wote wawe raia wa Tanzania
- Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi (CV) yenyenye Anuani na namba za simu majina matatu ya wadhamini.
- Waombaji wote wawe na kitambulisho cha **NIDA** au namba za kitambulisho
- Waombaji wote waambatanishe picha mbili za "Passport Size" za hivi karibuni na ziandikwe jina kwa nyuma.
- Watakaofalu kuitwa kwenye usaili majina au orodha yao itawekwa kwenye tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti ambayo ni www.kibitidc.go.tz
- **Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta**
- Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **15/07/2022**
- **Waombaji waliotuma maombi kwa Tangazo la awali, wasitume tena maombi.**

Maombi yatumwe kwa Anuani ifuatayo;

Mkurugenzi Mtendaji (W),
 Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti,
 S.L.P 33,
KIBITI.


 Msena N. Bina,
Kny: MKURUGENZI MTENDAJI (W),
KIBITI.



Nakala:-

Katibu,
 Ofisi ya Rais,
 Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
 Jengo la Dkt Asha Rose Migiro,
 S.L.P 2320,
DODOMA.

- " Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti www.kibitidc.go.tz
- " Mbao za matangazo - Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti.